# USAFIRI ARDHINI

Julai - Disemba, 2023

ISSN 2961 - 6255

Toleo Na. 02




## SAFARI SAA 24 RUKSA KUANZIA OKTOBA 1, 2023

Tathimini iliyofanyika imeonesha kuwa udhibiti wa hali ya usalama umeimarika kupitia Jeshi la Polisi, wananchi wanahifadhi pesa zao benki, LATRA imesimika mfumo madhubuti wa kufuatilia mwenendo wa magari (VTS)... Uk 27

## KAMATI YAIPONGEZA LATRA MFUMO WA VTS

Ziara hii Wajumbe wa Kamati wamejifunza namna mfumo wa VTS unavyofanya kazi, kimsingi mfumo huu ni muhimu kwani unasaidia madereva kubadilisha tabia zao (hatarishi)..... Uk 03

# Wahudumu wa Mabasi wadhaminiwa na LATRA

# TAHARIRI



Karibu katika toleo la pili la jarida la USAFIRI ARDHINI kutoka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Jarida hili limekusanya taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ambazo zimefanyika katika kipindi cha mwaka 2023 yaani kuanzia mwezi Julai, 2023 hadi Disemba 2023.

Lengo la jarida hili ni kukuhabarisha wewe mdau wetu kuhusiana na mambo ya msingi yanayotekelezwa na LATRA ikiwa ni sehemu ya utoaji wa elimu kuhusu shughuli za Mamlaka na masuala mbalimbali yanayogusa sekta ya Usafiri Ardhini.

Serikali ilitangaza rasmi safari za saa 24 kuanza rasmi Oktoba I, 2023 na Mamlaka ilitoa ratiba ya safari hizo kwa kushirikiana na watoa huduma, na ili kuboresha huduma hii Mamlaka iliwataka watoa huduma kuhakikisha Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) unafanya kazi muda wote, kutumia madereva waliosajiliwa na LATRA na kuhakikisha wanatumia Tiketi za Kielektroni na kuweka taarifa sahihi za abiria kwenye tiketi hizo.

Aidha, Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), aliyekuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, alizindua Bodi ya pili ya Wakurugenzi LATRA Julai 11, 2023 inayoongozwa na Prof. Ahmed Ame, Mwenyekiti wa Bodi hiyo na kuwaasa kusimamia Menejimenti ya LATRA vizuri pamoja na kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo .

Katika kipindi cha Mwezi Julai, 2023 LATRA iliwatunuku vyeti madereva 999 baada ya kufuzu mtihani wa kuthibitishwa na LATRA ambapo madereva hao walitunukiwa vyeti hivyo na Mhe. Atupele Mwakibete (Mb), aliyekuwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) katika ukumbi wa Arnatouglou Jijini Dar es Salaam Julai 1, 2023.

Juhudi za LATRA kuwathibitisha madereva hao ni kwa lengo la kuleta mapinduzi makubwa katika Sekta ya Usafiri Ardhini na kuimarisha usalama barabarani kwani kutakuwa na madereva makini waliothibitishwa na Mamlaka.

Vilevile Novemba 22, 2023 Mamlaka ilizindua rasmi mafunzo ya wahudumu wa vyombo vya moto kibiashara na kuwadhamini wahudumu 10 kutoka kampuni 10 za mabasi ya masafa marefu ili kusisitiza Kanuni ya kuwasajili wahudumu hao baada ya kuhudhuria mafunzo yatakayowawezesha kufahamu Sheria, Kanuni, taratibu na Kuwajali wateja kwani kufanya hivyo kutaboresha sekta ya usafiri nchini.

Katika kuendelea kuboresha sekta ya usafiri nchini, Mamlaka imeendelea kutoa elimu kwa wasafirishaji kuhusu kazi na majukumu yake kwa mujibu wa Sheria, kwa kufanya mikutano na wadau pamoja na kupokea maoni na changamoto zinazowakabili katika maeneo mbalimbali kama vile Mkoa wa Kigoma.

Hayo ni Baadhi tu ya mengi ambayo utayapata katika jarida hili la USAFIRI ARDHINI. Nami nitumie fursa hii kukukaribisha tena katika kurasa hizi ili upate kufahamu vizuri maendeleo ya Sekta ya Usafiri Ardhini na Udhibiti wa huduma za usafiri nchini, Nakutakia usomaji mwema.

***Pamoja kwa Usafiri Bora***



*CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA akikata Utepe kama ishara ya kufunguliwa rasmi kwa mafunzo ya wahudumu/makondakta wa vyombo vya moto kibiashara, Novemba 22, 2023, ofisi za LATRA - Dar es Salaam.*

# LATRA YADHAMINI WAHUDUMU 10 WA VYOMBO VYA MOTO KIBIASHARA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imedhamini kwa kulipa ada za mafunzo kwa wahudumu 10 wa vyombo vya moto kibiashara kutoka kwa kampuni 10 za mwanzo zilizowasilisha orodha ya wahudumu/makondakta waliokuwa tayari kuanza mafunzo yatakayotolewa na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) pamoja na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE).

Hayo yamebainishwa na CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA wakati wa hafla fupi ya uzinduzi wa mafunzo ya wahudumu/makondakta wa vyombo vya moto kibiashara iliyofanyika Novemba 22, 2023 katika ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam.

CPA Suluo amesema kuwa, wahudumu watano watapatiwa mafunzo hayo Chuo cha NIT na wengine watano chuo cha CBE na amewasihi wahudumu hao kuzingatia mafunzo ili kuongeza tija wanapotekeleza majukumu yao ya kuwahudumia abiria.

"Ninawasihi wahudumu/makondakta kuzingatia masomo yenu, msome kwa bidii na baada ya kufaulu mfike LATRA kwa ajili ya kusajiliwa. Usajili utafanyika kupitia mfumo wetu wa kidigiti (rrims.latra.go.tz) na kila muombaji atatakiwa kuwa na namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA), Cheti cha mafunzo kutoka CBE au NIT na Cheti cha Uchunguzi wa Afya ili aweze kusajiliwa," ameeleza CPA Suluo.

Aidha, CPA Suluo ameongeza kuwa, mkazo wa mafunzo hayo utawekwa kwenye kufahamu Sheria, Taratibu, Kanuni na Kujali Wateja (Customer Care), na Kanuni itayosisitizwa ni ile inayohusu Usajili wa Wahudumu ili wajue majukumu yao na pale wasipotimiza wafahamu wanatenda kosa lenye kustahili adhabu.

CPA Suluo amezitaja faida za wahudumu wa vyombo vya moto kibiashara kuhudhuria mafunzo na kisha kusajiliwa na Mamlaka ambazo ni; Wamiliki kupata wasimamizi mahiri na weledi wa kazi waliyopewa, Wahudumu kufanya kazi kwa weledi, umakini na ufanisi zaidi, Kuboresha huduma za usafiri ardhini hususan wa abiria nchini, Abiria kuvutiwa na huduma nzuri inayotolewa na kupata amani safarini, Kurasimisha kazi ya wahudumu iheshimike kama zilivyo kazi nyingine, Kulinda mitaji ya wamiliki wa vyombo na vipato vya wahudumu, Kuwezesha taasisi zinazoshughulikia masuala ya ajira

>>> Inaendelea UK 2

<<< Inatoka Uk 1

# LATRA YADHAMINI WAHUDUMU 10 WA VYOMBO VYA MOTO KIBIASHARA

kuwa na taarifa sahihi zinazowezesha kusimamia maslahi ya wahudumu katika ajira na Kuongeza nidhamu na uwajibikaji kwa wahudumu na watumiaji wa huduma.

Naye Bw. Priscus Joseph, Katibu Mkuu wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), amesema mafunzo hayo kwa wahudumu yanaenda kuboresha utoaji wa huduma kwa kuwa yanaenda kuongeza weledi na tija. Pia amewasihi wahudumu hao kuwakumbusha abiria ishara za kiusalama ndani ya mabasi, wawe karibu na madereva na kuwakumbusha kutoendesha chombo cha moto kwa mwendokasi pamoja na kuwakumbusha abiria kutokuwa na haraka ya kufika ili dereva aweze kufuata Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo pindi anapokuwa safarini.

Nao wakufunzi kutoka Chuo cha CBE na NIT wameishukuru LATRA kwa kuwashirikisha katika mchakato mzima wa uandaaji wa mtaala na uzinduzi wa mafunzo hayo na wamesema, "Tumejipanga vizuri kuwapatia mafunzo na tutatumia umahiri wetu na uzoefu tulionao katika kutoa mafunzo haya kwa wahudumu, ili kuhakikisha wanakuwa bora wanapotekeleza majukumu yao na kuifanya sekta ya usafiri ardhini kuwa yenye tija."

Mafunzo ya wahudumu/makondakta wa vyombo vinavyotoa huduma za usafiri kibiashara yatatolewa kwa kuzingatia mitaala ya CBE na NIT iliyozinduliwa rasmi na Mhe. Atupele Freddy Mwakibete aliyekuwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, tarehe 1 Julai, 2023.

# KAMATI YAIPONGEZA LATRA MFUMO WA VTS

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Mhe. Selemani Moshi Kakoso (Mb) pamoja na wajumbe wa Kamati hiyo, wameipongeza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kutumia Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) ambao umesaidia kupunguza ajali za mabasi ya masafa marefu nchini.

Pongezi hizo zimetolewa Septemba 9, 2023 jijini Dar es Salaam ambapo Wajumbe wa Kamati hiyo walipotembelea Kituo cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) na kujionea jinsi mfumo huo unavyofanya kazi.

Vilevile Mhe. Kakoso amesema kuwa, Serikali kupitia LATRA imewekeza katika mfumo huu ambao umekuwa na tija kwa kupunguza kwa kiasi kikubwa suala la ajali barabarani ukilinganisha na miaka ya nyuma kabla ya mfumo huo kuanza, ingawa sasa ni wakati wa kuuboresha zaidi maana teknolojia imebadilika.

Ameongeza kuwa, "Kamati imebaini kuwa LATRA wanafuatilia mfumo lakini bado kuna baadhi ya madereva na wanaofunga vifaa vya mfumo huu si waungwana kwa sababu wamekuwa wanaingilia mfumo ambapo athari zake tumekuwa tukiziona ikiwemo suala la ajali ambazo zimekuwa zikigharimu maisha ya watanzania. Hapa Kamati tunaitaka LATRA ikae pamoja na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na wadau wengine ili kuhakikisha kampuni hizo zinafuata Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo na kuzichukulia hatua pindi wanapozikiuka."

Wakati huohuo Mhe. Kakoso ameipongeza LATRA kwa kubuni mifumo ya kielekroni inayorahisisha utendaji kazi wa Mamlaka hiyo. "Kwanza niwapongeze sana LATRA, naamini mapinduzi makubwa ya kisayansi yaliyofanywa yakisimamiwa vizuri na serikali yanakwenda kuleta mabadiliko makubwa nchini, sambamba na hilo wasimamieni wamiliki wa magari ya masafa marefu ambao kwa mujibu wa kanuni wanatakiwa kuwa na

>>> Inaendelea UK 3



CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA akielezea namna LATRA inavyodhibiti Usafiri Ardhini kupitia Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu wakati Wajumbe wa Kamati hiyo walipotembelea Kituo cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS), Septemba 9, 2023

<<< Inatoka Uk 2

# KAMATI YAIPONGEZA LATRA MFUMO WA VTS

madereva wawili ili dereva asiendeshe gari kwenye hali ya uchovu, kwa atakaekiuka asimamishiwe leseni yake ya usafirishaji au kufungiwa kabisa kwa sababu nyie ndio mna mamlaka hayo kisheria" amesema Mhe. Kakoso.

Akizungumza mbele ya Wajumbe wa Kamati hiyo, Waziri wa Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb) amesema kuwa Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) ni wa muhimu kwani unasaidia kupunguza madhara ya ajali kwa kuepusha tabia hatarishi walizonazo madereva na hivyo kuhakikisha usalama wa basi na abiria waliopo ndani yake

"Katika ziara hii Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu wamejifunza namna mfumo wa VTS unavyofanya kazi, kimsingi mfumo huu ni muhimu kwani unasaidia madereva kubadilisha tabia zao (hatarishi), madereva wanapaswa waelewe kuwa vyombo vyao vimebeba abiria hivyo usalama kwao iwe ni kitu cha kwanza," ameongeza Mhe. Prof. Mbarawa.

Naye CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA ameishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kutembelea LATRA na kujifunza kuhusu shughuli za kiudhibiti huku akielezea mwelekeo wa LATRA katika kudhibiti makampuni yanayohusika na ufungaji wa vifaa vya kufuatilia mwenendo wa magari (VTD).

"Napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwani hii ni mara ya kwanza imetutembelea na kujifunza mambo mbalimbali ikiwemo mfumo mzima wa VTS unavyofanya kazi pamoja na changamoto zake, kikubwa wameweza kufahamu kuwa makampuni yanayofunga vifaa hivi hayadhibitiwi moja kwa moja, hivyo hata inapotokea kuchezewa kwa mifumo mara nyingi anayeadhibiwa ni mmiliki pekee, kanuni zimeshatungwa na Mhe. Waziri Prof. Mbarawa ametueleza kuwa zipo katika hatua za mwisho hivyo hivi karibuni zitakuwa tayari na itatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu," amesema CPA. Suluo.

# MABASI 36, MADEREVA 10 WAFUNGIWA KWA KUKIUKA MASHARTI YA LESENI




*Huduma za Usafiri wa mabasi ya masafa marefu zikiendelea katika Kituo Kikuu cha Mabasi Magufuli*

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imesitisha leseni za mabasi 36 kutokana na makosa mbalimbali ikiwemo kuingilia Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) na kupelekea mwendokasi hatarishi kinyume na Sheria za Usalama barabarani kufuatia tathmini iliyofanyika ya mabasi hayo yanayofanya safari za masafa marefu kwa saa 24.

Hayo yamesemwa na CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA wakati Akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano uliofanyika ukumbi wa mikutano ofisi ya LATRA Mkoa wa Dar es Salaam Novemba 9, 2023 kuhusu tathmini ya mabasi yaliyopewa ratiba za safari za usiku kuanzia Oktoba mosi mwaka huu.

Akizungumza na wanahabari CPA Suluo amesema kuwa asilimia kubwa ya mabasi yaliyopewa ratiba za kufanya safari usiku yanakiuka Sheria za Usalama Barabarani na Masharti ya Leseni zao, hivyo imepelekea Mamlaka kuchukua hatua.

"Kufuatia tathmini ya safari za saa 24 tumebaini kati ya mabasi 246 ambayo yamepewa ratiba za kufanya safari za usiku, 80% ya mabasi hayo (Mabasi 197) yanaendeshwa mwendo hatarishi kati ya kilomita 86-89 kwa saa, na 09% ya mabasi hayo yanaendeshwa mwendo hatarishi zaidi kati ya kilomita 90-103 kwa saa, hivyo LATRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi tumechukua hatua yakusitisha leseni za Mabasi 36 mpaka Mamlaka itakapo jiridhisha kuwa kampuni hizo zimejirekebisha" Amesema CPA Suluo.

Aliongeza kuwa, tathmini hiyo imeonesha kuna baadhi ya wasafirishaji hawatekelezi utaratibu ulioelekezwa na Kanuni za leseni za usafirishaji kwa magari ya abiria kutumia madereva wawili kwa safari za njia ndefu zinazozidi kilomita 700, ambapo baadhi ya madereva huepuka matumizi ya kitufe cha utambulisho (i - Botton) ambacho ni muhimu ili kuiwezesha Mamlaka kumtambua dereva na muda aliokuwa anaendesha gari husika.

"Katika ufuatiliaji wetu, tumebaini baadhi ya madereva wanafanya safari ndefu bila kuwa na dereva wa pili, na kuna madereva wanafika saa nne usiku, wanapumzika kwa saa chache na kuanza safari nyingine usiku huo huo" Alisema

>>> Inaendelea UK 5

<<< Inatoka Uk 4

# MABASI 36, MADEREVA 10 WAFUNGIWA KWA KUKIUKA MASHARTI YA LESENI

Aidha, CPA Suluo alisema kuwa ni lazima wamiliki wa mabasi wahakikishe wanatoa tiketi za kielektroni zenye taarifa za msingi na sahihi za abiria ili kuhakikisha kila abiria anayesafiri anatambulika na kumuwezesha kupata haki zake endapo atakumbana na kadhia yeyote.

“Suala la kuandika taarifa za msingi na sahihi za abiria ni la lazima, na sio tu kwa wanaofanya safari za usiku, hii inawagusa wote, na haitakiwi taarifa hizi ziandikwe kwa mkono, tunaelekea kusaini Mkataba wa Maelewano (MOU) na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ili kuwasaidia wananchi kupata stahiki zao wanapopata ajali, bila ya taarifa hizi itakuwa ngumu kufanikisha hilo” Ameongezea CPA Suluo.

Kwa upande wake SACP Ramadhan Ng’anzi, Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani ametangaza kufungiwa leseni za madereva 10 ambao wamebainika kukiuka Sheria za Usalama Barabarani na kuhatarisha maisha ya abiria na mali zao, na kuwa baada ya kutumikia kifungo cha leseni zao hawatarejeshewa leseni hizo hadi watakapofuata utaratibu wa kusailiwa na kupata leseni.

“Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani limefungia leseni za maderva 10 na hawataruhusiwa kuendesha gari lolote kwa kipindi chote cha kutumikia adhabu, hatutovumilia madereva wanaokiuka Sheria, kwa kushirikiana na Mamlaka tumefungia leseni za madereva hao na wengine kufikishwa mahakamani pamoja na kufutiwa leseni kwa kosa la kuingilia Mfumo wa VTS na kwenda mwendo kasi unao hatarisha maisha ya binadamu na mali zao” Amesema SACP Ng’anzi.

Naye Bw. Priscus Joseph, Katibu Mkuu wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) amewaasa madereva na wamiliki kufuata Sheria za Usalama Barabarani pamoja na Masharti ya leseni zao huku akiiomba LATRA na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kukishirikisha chama hicho wakati wa kuchukua hatua.

“Niwasihi tu madereva na wamiliki wenzangu wa mabasi tuendeshe kwa mwendo unaotakiwa, hata kwa mwendo chini ya kilomita 80 kwa saa hasa katika kipindi hiki cha mvua, hata hivyo siku hizi tuna hadi safari za usiku hivyo sioni sababu itakayotufanya tushindane. Hivyo, tuendelee kutii Sheria, pia naomba LATRA kutushirikisha juu ya taarifa ya kufungia mabasi kabla ya kuchukua hatua za kisheria.” Amesema Bw. Joseph.

Kwa upande wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA CCC) limeishukuru LATRA na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kwa kusimamia vyema usalama wa usafiri ardhini na limewashauri watoa huduma wa usafiri kuzingatia usalama wa abiria, na usalama wa vyombo vya usafiri ili kuwezesha huduma za Usafiri kuwa endelevu.



# MABASI 38 YA ‘NEW FORCE ENTERPRISES’ YAFUTIWA RATIBA ZA ALFAJIRI




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) CPA Habibu Suluo amesema mabasi 38 kampuni ya New Force Enteprises yamefutiwa ratiba za alfajiri ambapo mabasi 10 ni yale yanayoanza safari saa 9.00 alfajiri na mabasi 28 yanayoanza safari saa 11.00 alfajiri. Aidha, kuanzia tarehe 5 Julai, 2023, mabasi hayo yatafanya safari zao kuanzia saa 12.00 asubuhi na kuendelea.

Akizungumza na waandishi wa habari Julai 3, 2023 katika Ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam, CPA Suluo amesema uamuzi huo umefikiwa kutokana na kuwapo kwa uvunjaji wa Kanuni za Usafirishaji wa Magari ya Abiria, 2020 pamoja na matukio ya ajali ya mabasi hayo ambapo ndani ya takribani wiki nne; kati ya tarehe 6 Juni, 2023 na 2 Julai, 2023 mabasi ya kampuni ya New Force yamehusika katika ajali tano na sababu kubwa ni uzembe wa madereva wa mabasi hayo.

CPA Suluo ameongeza kuwa, uchunguzi wa awali uliofanywa na Mamlaka ulibaini kuwepo kwa uvunjaji wa makusudi wa Kanuni za Usafirishaji wa Magari ya Abiria, 2020 hususan kutumia ratiba za saa 9.00 alfajiri na saa 11.00 alfajiri zinazomtaka dereva anayeendesha basi la abiria kutumia kifaa cha utambuzi (i - B–utton).

Vilevile amesema Kampuni ya New Force ni miongoni mwa watoa huduma waliopewa ratiba za saa 09.00 alfajiri na saa 11.00 alfajiri ambapo walipewa sharti la kuhakikisha madereva watakaondesha mabasi kwa ratiba hizo ni wale waliothibitishwa na LATRA na kupatiwa kitufe cha utambuzi (ibutton) ambapo wanapaswa kutumia kifaa hicho ili waweze kufuatiliwa kupitia Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Mabasi (VTS) pindi yanapokuwa safarini.

Naye Bw. Masumbuko Masuke, Meneja wa Kampuni ya New Force Enterprises amesema, “Tunafahamu hizi ajali zinagharimu maisha ya Watanzania pamoja na miundombinu iliyopo, tunaahidi kubadilika kwa kuwapeleka madereva wetu kufanya mtihani ili wathibitishwe na tutahakikisha tunawasimamia katika kufuata Sheria za Usalama Barabarani ili kuepusha ajali na hasara zinazojitokeza,”

Kwa upande wake, Bw. Leo Ngowi Katibu wa Baraza la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA-CCC) amewataka abiria kupaza sauti zao na kutoa taarifa kwa Mamlaka husika (LATRA na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani) pindi wanapoona kuna vitendo hatarishi vinavyofanywa na dereva pindi wanapokuwa safarini na pia ameipongeza Mamlaka kwa hatua sahihi waliyochukua kwa kuwa inaonesha jinsi Mamlaka inavyojali watumia huduma na watoa huduma za usafiri ardhini.

# MHE. MTAKA AIPONGEZA LATRA




***Mhe. Anthony Mtaka, Mkuu wa Mkoa Njombe, akitoa maoni yake baada ya kutembelea banda la LATRA katika Maonesho ya Kimataifa ya Wakulima Nanenane viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya, Agosti 5, 2023***

Mhe. Anthony Mtaka, Mkuu wa Mkoa Njombe, ameipongeza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kusaidia kuondosha malalamiko yasiyo ya msingi kwa wasafirishaji nchini na kuleta suluhu badala ya malumbano.

Mhe. Mtaka ameyasema hayo Agosti 5, 2023 alipotembelea banda la LATRA katika Maonesho ya Kimataifa ya Wakulima Nanenane viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya.

Aidha, Mhe. Mtaka ameipongeza LATRA kwa kujitangaza ndani ya muda mfupi tangu kuanzishwa kwake ambapo imekuwa miongoni mwa taasisi zenye hadhi kubwa nchini kutokana na namna inavyotekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi.

Vilevile Mhe. Mtaka ameisihi LATRA kuwekeza kwenye ubunifu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa kuwatumia vijana ili kutengeneza mifumo itakayorahisisha zaidi utendaji kazi na utoaji wa huduma za usafiri ardhini kwa kuwa teknolojia inaleta suluhisho katika masuala mbalimbali ya kiutendaji.

Katika hatua nyingine, Mhe. Mtaka ameitaka LATRA kuwa washauri wazuri kwenye miundombinu mipya inayojengwa na Serikali kwenye maeneo ya usafiri. Pia ameshauri kwenye maeneo ya stendi pale abiria wanaposubiri waone masuala ya msingi yanayohusu usafiri kwa njia ya mtandao.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu LATRA CPA Habibu Suluo, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA Bw. Salum Pazzy, alimshukuru Mhe. Mtaka kwa miongozo aliyoitoa na kuwa Mamlaka imeshafunga runinga maalumu katika Kituo cha Mabasi Magufuli na Kituo cha Nanenane Dodoma kwa ajili ya kuonesha taarifa mbalimbali za abiria.

# ALLY'S STAR NA KATARAMA LUXURY KUANZA SAFARI ALFAJIRI




Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imerejesha ratiba za mabasi tisa (9) ya Kampuni ya Ally's Star yenye namba za usajili T946EBF, T947EBF, T948EBF, T354DXS, T357DXS, T360DXS, T233EBG, T232EBG na T178DVB na mabasi matatu (3) ya Kampuni ya Katarama Luxury yenye namba za usajili T835EBR, T836EBR na T212ECR. Basi la Ally's Star litaanza safari saa tisa kamili (9:00) alfajiri na Katarama saa kumi kamili (10:00) alfajiri kuanzia Agosti 12, 2023 ili kuepusha mashindano yasiyo na tija kwa kukimbizana kuwahi kufika.

Hayo yamebainishwa na Bw. Salum Pazzy, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kutoka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) alipozungumza na waandishi wa habari Agosti 11, 2023 katika ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam.

"Mamlaka imekua ikifuatilia utoaji wa huduma za wasafirishaji hawa kwa ukaribu kupitia wataalam wetu nchi nzima ikiwa ni pamoja na uzingatiaji wa ratiba yaani muda wa kuanza safari, utumaji wa taarifa katika mfumo wa kufuatilia mwenendo wa magari, mwendokasi wa mabasi na matumizi ya kitufe cha utambuzi wa dereva (i - Button). Baada ya kuona kuwa wamejirekebisha ndio tumeamua kuwarejeshea ratiba hizo," amesema Bw. Pazzy.

Vilevile amesema kuwa, LATRA imekua ikitoa elimu kwa wafanyakazi na wamiliki wa kampuni hizo ikiwa ni pamoja na matumizi ya Mfumo wa kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) pamoja na kufanya vikao vya pamoja na wamiliki wa makampuni hayo ambapo wametoa ahadi ya kuongeza ufuatiliaji wa mabasi yao.

Aidha, Bw. Pazzy ameeleza kuwa, uamuzi huo ni kwa mujibu wa kifungu cha 5(1) (b) na 6(b) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413 na Kanuni za Leseni za Usafirishaji Magari ya Abiria za Mwaka 2020 ambapo pamoja na mambo mengine, LATRA ina jukumu la kutoa,

>>> Inaendelea UK 9


<<< Inatoka Uk 8

# ALLY'S STAR NA KATARAMA LUXURY KUANZA SAFARI ALFAJIRI

kuhuisha na kufuta vibali na leseni za usafirishaji, na kukuza usalama wa sekta zinazodhibitiwa ikiwa ni pamoja na usalama wa watumiaji wa huduma.

Naye Bw. Abdallah Maulid Abdallah, Mtendaji Mkuu kutoka basi la Ally's Star na Bw. Elimboto Njoka Mtatuu, Meneja Uendeshaji Kutoka Katarama Luxury wamemshukuru CPA Habibu Suluo na Uongozi wa LATRA kwa ushirikiano walioonesha na wameahidi kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za Usalama Barabarani ili kuwa na usafiri ardhini ulio bora na salama.

Ikumbukwe kuwa, tarehe 19 Juni, 2023 Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ilisitisha ratiba ya mabasi ya Ally's Star na Katarama Luxury kuanza safari saa tisa (9:00) alfajiri na saa kumi na moja (11:00) alfajiri na kupewa ratiba ya kuanza safari saa kumi na mbili (12:00) asubuhi. Hatua hiyo ilitokana na Mamlaka kupata taarifa na kuthibitisha uwepo wa mabasi ya kampuni hizo yanayokwenda mikoani kuchezea Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) na hivyo kusababisha kusafiri kwa mwendo kasi kwa lengo la kufanya mashindano ya kuwahi kufika kwenye vituo/stendi za mabasi.



# KAHATANO: WASILISHENI MAOMBI YA HUDUMA ZA USAFIRI WA SAA 24




*Bw. Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara - LATRA akizungumza na waandishi wa habari kuhusu lengo la kuwaalika wasafirishaji wenye nia ya kufanya safari saa 24 kutuma maombi ya ratiba hizo, Agosti 18, 2023 katika ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam.*

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetoa rai kwa wamiliki wa mabasi ya masafa marefu nchini wenye nia ya kutoa huduma za usafiri kwa saa 24 kuwasilisha maombi yao ili muda wa kuanza safari hizo utakapoanza rasmi iwe rahisi kufahamu mahitaji halisi ikiwa ni pamoja na maeneo yanayotakiwa kupatiwa huduma hiyo.

Hatua hiyo ni katika kutekeleza agizo alilolitoa Mhe. Kassim Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Juni 28, 2023 kuhusu kuanza kwa safari za usiku kwa mabasi ya masafa marefu nchini.

Hayo yamebainishwa na Bw. Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara alipozungumza na waandishi wa habari Agosti 18, 2023 katika ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam.

Akizungumza kwa niaba ya CPA Habibu Suluo- Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Bw. Kahatano amesema kuwa, Juni 28, 2023 Serikali kupitia Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitoa maagizo kwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuweka utaratibu wa mabasi kuanza kutembea saa 24 na tayari taratibu za kutekeleza maagizo zimeanza.

Wakati huohuo, Bw. Kahatano amezitaka kampuni zilizoanza kutoa huduma za usafiri kinyume na ratiba zao kuacha kufanya hivyo kwa kuwa wanaenda kinyume na Kanuni zilizopo, “Hivi karibuni yamejitokeza baadhi ya makampuni yanazotoa huduma nje ya ratiba ambazo yamepatiwa na yameanza safari za usiku kwenda maeneo mbalimbali jambo ambalo ni kinyume na Kanuni kwa maana kila gari linatakiwa kufuata ratiba yake.”

Ameongeza kuwa, “Tumebaini kuna changamoto zimejitokeza kwa baadhi ya mabasi kuharibika usiku wa manane na mengine kuendeshwa mwendokasi kwa kuwa wanafahamu njiani hakuna udhibiti mkubwa wa askari polisi, kwa kawaida tukibaini matukio hayo kupitia mifumo yetu, huwataarifu polisi ili wachukue hatua, kwa kuwa muda wa usiku polisi huwa ni wachache, madereva wanatumia nafasi hiyo kufanya wanavyotaka jambo ambalo linahatarisha maisha ya abiria wanaopanda mabasi hayo.”

Vilevile Bw. Kahatano ametoa wito kwa wananchi, “Wananchi ambao wanapanga kusafiri usiku wajue kuwa huduma hizi hazijaanza rasmi hivyo wawe na subira vinginevyo watakuwa wanajaribu kuhatarisha maisha yao na wanaweza kukumbana na usumbufu pale mabasi hayo yatakapodhibitiwa njiani.”



*Mhe. Atupele Fredy Mwakibete (Mb), Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) akigawa cheti cha kuthibitishwa kwa mmoja wa madereva 999 waliofanya mtihani na kuthibitishwa na LATRA katika hafla ya uzinduzi wa Mtaala na Utoaji wa Vyeti, katika ukumbi wa mikutano wa Arnaoutoglou, Dar es Salaam, Julai 01, 2023.*

# MHE. MWAKIBETE AWAPONGEZA MADEREVA 999 WALIOTHIBITISHWA NA LATRA

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) Mhe. Atupele Fredy Mwakibete (Mb) amewapongeza madereva 999 waliofanya mtihani na kuthibitishwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) na amewasihi ambao hawakufaulu kutokata tamaa bali wajikumbushe tena yale waliyojifunza na warudi kufanya mitihani ili wathibitishwe.

Mhe. Mwakibete amesema hayo kwenye ufunguzi wa hafla ya uzinduzi wa Mtaala na Utoaji wa Vyeti kwa Madereva wa Vyombo vya Moto Vinavyotoa Huduma Kibiashara Waliothibitishwa na LATRA iliyofanyika Julai 01, 2023 katika ukumbi wa mikutano wa Arnaoutoglou, Dar es Salaam.

"Ninaamini hata wale ambao hawakufaulu, wamejikumbusha mambo kadhaa na niwasihi wasikate tamaa bali wajikumbushe tena yale waliyojifunza na warudi kufanya mitihani hii ili wathibitishwe na tuje kuwapatia vyeti siku chache zijazo," ameeleza Mhe. Mwakibete.

Vilevile amesema kuwa, juhudi za LATRA za kuthibitisha madereva zitaleta mapinduzi makubwa katika sekta ya usafiri ardhini nchini kwa kubadili tabia za madereva wakiwa barabarani na kutakuwa na tofauti ya dereva aliyethibitishwa na LATRA na yule ambaye hakuthibitishwa na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha usalama wa sekta ya usafirishaji.

Aidha, Mhe. Mwakibete amezungumzia faida za kuwathibitisha madereva, "Serikali inaamini kuwa hadhi ya madereva itaongezeka, wataheshimika zaidi na maslahi yao yataboreshwa na zaidi, taaluma hii ya udereva itarasimishwa na kuwaongezea madereva thamani kwenye masoko ya ajira ya ndani na nje ya nchi, hususan kwenye nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Soko la Pamoja la Mashariki na Kusini mwa Afrika (COMESA) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC)," amefafanua Mhe. Mwakibete.

Naye Mhe. Jumanne Sagini (Mb), Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi na Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani amesema zaidi ya asilimia 76 ya ajali zinazotokea barabarani zinasababishwa

>>> Inaendelea UK 12

>>> Inatoka UK 11

# MHE. MWAKIBETE AWAPONGEZA MADEREVA 999 WALIOTHIBITISHWA NA LATRA

na makosa ya kibinadamu na hivyo amewaasa madereva hao kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Usalama Barabarani ili kupunguza na kuondoa kabisa ajali hizo.

Vilevile, ameipongeza LATRA kwa kuendelea kushirikiana na taasisi nyingine za umma ikiwemo Jeshi la Polisi, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) na VETA kwa kuandaa kwa pamoja maswali yenye nia njema ya kufahamu uelewa wa madereva wa vyombo vya moto vinavyotoa huduma kibiashara.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, CPA Habibu Suluo amesema Kanuni ya 22(i) ya Leseni za Usafirishaji (Magari ya Abiria), 2020 inaainisha moja ya masharti ya leseni zinazotolewa na LATRA ambapo inawataka wenye vyombo vya moto vinavyotoa huduma za usafiri kibiashara, kuhakikisha kila dereva anayeendesha vyombo hivyo wanakuwa na Cheti cha Uthibitisho kinachotolewa na Mamlaka baada ya kufanya mtihani na kufaulu,

Vilevile amesema kuwa, kabla ya kuanza kutahini madereva, Mamlaka kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, ilipitia maswali ya mtihani yanayotumika kwenye vyuo vinavyozalisha madereva nchini kulingana na mitaala inayotumika na kuyaweka katika mfumo wa Kutahini Madereva (DTS).

Aidha, CPA Suluo ameeleza kuwa, maswali hayo yanawapima madereva kuhusu uelewa wao kwenye maeneo ya alama na miongozo mbalimbali inayowasaidia kuendesha vyombo vya moto kwa usalama, “Baada ya maswali kupitishwa na kuwekwa kwenye mfumo, tarehe 1 Juni, 2022 Mamlaka ilianza rasmi kutumia mfumo wa DTS kutahini madereva ambapo hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2023 jumla ya madereva 1,744 walikuwa wamefanya mtihani na madereva 999 walifaulu.”

“Kwa kuwa tunawajali madereva wetu na tunataka wafaulu kwa wingi, LATRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, tumeandaa video mbalimbali zinazoelimisha kuhusu masuala ya msingi ya kuzingatia ukiwa barabarani ikiwemo suala la alama. Video hizi zinapatikana katika Online TV ya Mamlaka inayopatikana kwa jina la latraTV kwenye mtandao wa YouTube, hivyo ninawasihi wakatazame ili kujielimisha zaidi kabla ya kuja kufanya mtihani,” amesema CPA Suluo



*Mhe. Prof. Makame Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi, akizungumza na madereva waliofika ofisi za LATRA Dar es Salaam ili kufanya mtihani na kuthibitishwa kwa Mujibu wa Sheria*

# LATRA YATOA ONYO YA TAHADHARI KWA 'NEW FORCE ENTERPRISE'




Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetoa onyo ya tahadhari kwa Kampuni ya New Force kutokana na kuwa na matukio mengi ya ajali ambapo tarehe 7 Agosti, 2023 basi Na. T618DMG lilipata ajali kati ya maeneo ya Ruahambuyuni na Mikumi na sababu ya ajali hiyo ilikuwa ni uzembe wa dereva kutaka kuyapita magari mengine bila kuchukua tahadhari.

Hayo yamesemwa na Bw. Salum Pazzy, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kutoka LATRA alipozungumza na waandishi wa habari Agosti 11, 2023 katika ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam.

Ameongeza kuwa, "hali ya kuendelea kuwepo na matukio ya ajali za barabarani kutokana na uzembe wa madereva katika kampuni ya New Force haikubaliki. Hivyo, Mamlaka inatoa nafasi kwa kampuni hiyo kutafuta suluhisho la sababu za ajali hizo haraka na Mamlaka itaendelea kuifuatilia kampuni hiyo kwa ukaribu. Vinginevyo, Mamlaka haitasita kuchukua hatua zingine za kisheria ikiwa ni pamoja na kufuta leseni za usafirishaji za kampuni hiyo."

Ikumbukwe kuwa, mnamo tarehe 3 Julai, 2023 Mamlaka ilisitisha ratiba za mabasi 38 ya kampuni hiyo kuanza safari zake saa tisa (9:00) alfajiri na saa kumi na moja (11:00) alfajiri ikiwa ni sehemu ya hatua za kupunguza ajali za barabarani katika kampuni hiyo. Aidha, adhabu hiyo ilitokana na kuwepo kwa mfululizo wa ajali katika kipindi cha wiki nne mfululizo.

Katika hatua nyingine, LATRA imezionya kampuni za mabasi za Kilimanjaro Truck Company Limited, Abood Bus Service, Baraka Classic, Kapricon, Frester na Nyehunge Express kwa kuendelea kukiuka Sheria, Kanuni na Taratibu za usafirishaji.






<<< *Wafanyakazi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) katika semina ya Afya itakayochagiza kuboresha ufanisi wawapo kazini.*
*Semina hiyo imefanyika ofisi za LATRA Dar es Salaam, Disemba 2, 2023.*

*CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu (LATRA) akiambatana na Wakuu wa taasisi na viongozi mbalimbali wa Serikali Kukabidhi hundi ya mfano yenye thamani ya Shiingi Bilioni mbili kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ikulu Chamwino - Dodoma, Disemba 10, 2023. Ikiwa ni mchango kwa ajili ya waathiriwa wa maafa ya mafuriko Hanang - Manyara* >>>



# PROF. MBARAWA AITAKA BODI YA WAKURUGENZI LATRA KUISIMAMIA MENEJIMENTI YA MAMLAKA



*Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (wa Kwanza Kulia) akizungumza na Wajumbe wa Bodi ya LATRA, Menejimenti, Wafanyakazi na wanahabari katika uzinduzi wa Bodi ya pili ya Wakurugenzi ya LATRA, Julai 11, 2023, ofisi za LATRA Dar es Salaam.*

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb) ameitaka Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kuisimamia Menejimenti ya Mamlaka hiyo ili itekeleze vyema majukumu yake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo.

Mhe. Prof. Mbarawa amesema hayo alipokuwa akizindua Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inayoongozwa na Mwenyekiti Prof. Ahmed Mohamed Ame pamoja na wajumbe wengine sita akiwemo, Bi. Neema Joseph Ringo, Bw. Nuru Mohamed Ngoma, Mha. Michael Paul Kisaka, Bw. Allen Thobias Marwa, Wakili Tumaini Elisamia Silaa pamoja na Mha. Lucian Mafikiri Henry Kilewo

Uzinduzi wa Bodi hiyo umefanyika Julai 11, 2023 katika ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wajumbe wa Bodi mpya, waliomaliza muda wake, Menejimenti ya LATRA pamoja na waandishi wa habari.

"Jukumu kubwa la Bodi ni kuisimamia Menejimenti, sio kufanya kazi za Menejimenti. Bodi ipate mafunzo ya kutosha (Induction Program) na kufanya ziara za kujifunza ili kutekeleza vyema majukumu yake," ameeleza Prof. Mbarawa.

Vilevile, Mhe. Mbarawa ameielekeza Bodi hiyo kusimamia mapato na matumizi ya Mamlaka na kuhakikisha mchango wa asilimia 15 ya mapato ghafi yanawasilishwa kwenye Mfuko wa Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria na taratibu zilizopo.

Aidha, maelekezo mengine aliyoyatoa Mhe. Prof. Mbarawa kwenye hotuba yake ni pamoja na Kuweka utaratibu wa Mamlaka kukutana na wadau wake kila mwaka na kutoa elimu juu ya shughuli za Mamlaka pamoja na kushirikisha kikamilifu wadau wa Mamlaka hususan sekta binafsi kabla ya Mamlaka haijafanya maamuzi yanayoathiri utoaji wa huduma zinazodhibitiwa,

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) Bw. Gabriel Migire, Bw. Ahmed Mbegu amewapongeza wajumbe wa Bodi iliyomaliza muda wake kwa kuiwezesha LATRA kupata mafanikio yaliyopo

>>> Inaendelea UK 16

>>> Inatoka UK 15
na amesema ofisi ya Katibu Mkuu Uchukuzi inaiahidi Bodi mpya kupata ushirikiano pale utakapohitajika.

Naye Mkurugenzi Mkuu LATRA CPA Habibu Suluo amemshukuru Mhe. Mbarawa kwa kuzindua Bodi ya Wakurugenzi na ameahidi kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo huku akizingatia kwa weledi, umahiri na mshikamano na Bodi hiyo pamoja na wadau wote wa sekta ya udhibiti usafiri ardhini nchini.



# LATRA, POLISI KUONGEZA UDHIBITI WA AJALI NCHINI

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inategemea kuongeza na kudumisha ushirikiano uliopo kati yake na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani ili kuhakikisha udhibiti wa usalama barabarani unakuwa thabiti na wenye tija kwa watumiaji wa huduma za usafiri ardhini.

Hayo yamesemwa na Bw. Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara kutoka LATRA katika semina ya mafunzo kwa Wakuu wa Usalama Barabarani Mkoa (RTOs) na Wakaguzi wa magari nchini, semina hiyo ya siku tatu imefanyika katika ukumbi wa mikutano wa kampuni ya Superdoll Julai 17, 2023 na kufunguliwa na CP Awadhi H. Awadhi, Kamishna wa Operesheni na Mafunzo Tanzania.

Akizungumza baada ya kufunguliwa kwa mkutano huo, Bw. Kahatano amesema, “Kwakuwa elimu inayotolewa hapa inawafikia moja kwa moja Wakuu wa Usalama Barabarani Mkoa ambao ndio wasimamizi wakuu katika Mikoa yote Tanzania, pia wapo wakaguzi ambao ni watendaji, hii itasaidia kuongeza udhibiti wa usalama barabarani kwa kiasi kikubwa,” amesema Bw. Kahatano.

Aidha, Bw. Kahatano ameeleza kuwa ushiriki wa LATRA katika semina hiyo itaongeza ushirikiano ambao umekuwepo kwa muda mrefu kati ya LATRA na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani na hivyo kuleta tija katika utendaji.

“Ni mategemeo yangu kuwa ushirikiano uliopo baina yetu na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani utaongezeka zaidi baada ya semina hii, kwani tumepata fursa nzuri ya kuwezesha mafunzo haya na pia tunapata nafasi ya kueleza majukumu yetu kama LATRA na maeneo ambayo tunahusiana moja kwa moja na Jeshi la polisi,” ameeleza Bw. Kahatano.

Kwa upande wake CP Awadhi H. Awadhi ameishukuru LATRA pamoja na wadau wengine ambao wameshiriki kuwezesha semina hii ya mafunzo kwa Wakuu wa Usalama Barabarani Mkoa (RTOs) na wakaguzi wa Magari nchini.

“Nipende kutumia fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza LATRA pamoja na wadau wengine kama TIRA na TRA ambao muda wote wamekuwa wakishirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani ili kuhakikisha kwa pamoja tunadhibiti usalama barabarani, pia kwa kutuwezesha ili kufanikisha utoaji wa mafunzo haya kwa Wakuu wa Usalama Barabarani Mkoa (RTOs) na wakaguzi wa Magari nchini,” amesema CP Awadhi.

Lengo la semina hiyo ni kuwaongezea ujuzi wa ukaguzi wa vyombo vya moto na ufuatiliaji wa hali ya usalama kwa Wakuu wa Usalama Barabarani Mkoa (RTOs) na wakaguzi wa Magari nchini ili kuhakikisha uwezekano wa kupata ajali unapunguzwa kwa kiasi kikubwa.

# BODI YA WAKURUGENZI NA MENEJIMENTI YA LATRA WAPIGWA MSASA AFYA YA AKILI



*Dkt. Garvin Kweka kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, akielezea jambo kwa Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya LATRA pamoja na Menejimenti katika Semina maalum iliyoandaliwa na LATRA ili kupatiwa elimu ya Afya ya Akili, , Julai 27, 2023, Ukumbi wa mikutano ofisi ya LATRA Dar es Salaam*

Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) pamoja na Menejimenti wametakiwa kuzingatia Afya zao ikiwemo Afya ya Akili ili kutoathiri utendaji kazi wao wawapo kazini.

Hayo yamesemwa na Prof. Ahmed Mohamed Ame, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya LATRA, Jijini Dar es Salaam katika semina maalum iliyoandaliwa na LATRA kwa ajili ya Wajumbe wa Bodi ya LATRA na Menejimenti ili kupatiwa elimu ya Afya ya Akili iliyofanyika katika Ukumbi wa mikutano wa ofisi ya LATRA Mkoa wa Dar es Salaam, Julai 27, 2023.

Akizungumza na wajumbe wa Semina hiyo, Prof. Ame amewasisitiza kujitambua wakiwa katika hali ya msongo wa mawazo na kutafuta msaada wa kitaalamu kama ilivyoshauriwa na Mkufunzi wa Semina hiyo Dkt. Garvin Kweka, kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili.

“Binafsi najijua, kama nikiona tabia yangu ya ulaji imebadilika, mathalan hamu ya kula kuongezeka basi najua kuwa nina shida, haraka namuona daktari. Hivyo niwasihi tuu kama alivyoshauri daktari ukiona hauko sawa iwe ni msongo wa mawazo au shida nyingine ambayo inaweza kuathiri utendaji kazi wako muone mtaalamu ili upate msaada,” amesema Prof. Ame.

Kwa upande wake Dkt. Garvin Kweka, mkufunzi wa semina hiyo kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, wakati akiendelea na mafunzo hayo amesema kuwa vipo viashiria mbalimbali ambavyo vinawezea kusaidia kutambua kuwa mtu binafsi hauko sawa au jirani yako hayuko sawa, na hii itasaidia kuepusha athari zinazoweza kusababishwa na matatizo kwenye afya ya akili.

“Yapo mambo mengi ambayo yanaweza kukuonesha kuwa hauko sawa, au mtu mwingine hayuko sawa, kiashiria kikubwa ni mabadiliko ya tabia kwa ghafla, mathalan mtu huwa ni mcheshi sana lakini anakuwa mkimya ghafla, hii inaashiria kuna kitu kinamsumbua, sasa kwa kulijua hilo mnaweza kuchukua hatua za ziada ili kumsaidia kuwa sawa hivyo kupunguza uwezekano wa kuchukua hatua za kujidhuru,” amesema Dkt. Kweka.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Afya ya Akili ni ile hali ambapo akili ya mtu inaweza kuhimili hali ya maisha inayoweza kuleta msongo wa mawazo, kutumia vyema uwezo wake, kufanya kazi na kujifunza vizuri na kumfanya mtu kuishi vizuri kutokana na misingi ya jamii yake. Hii hutambuliwa

>>> Inaendelea UK 18

>>> Inatoka UK 17

na namna mtu anaweza kuitikia hisia zake.

Afya ya Akili isipokuwa sawa inaweza kusababisha msongo wa mawazo ambao unaweza kuleta athari mbalimbali kama vile migogoro ya kifamilia, kupungua kwa ufanisi katika shughuli mbalimbali, matumizi ya mihadarati, matatizo ya uhusiano na hata kutengwa na jamii, na matokeo yake yanaweza kusababisha mtu kujidhuru, hivyo ni vyema kila mmoja kutilia mkazo suala la Afya ya Akili ili kuhakikisha jamii inakuwa salama na uzalishaji unakuwa endelevu.




# MHE. MWAKIBETE: LATRA ENDELEENI KUCHUKUA HATUA

Mhe. Atupele Fred Mwakibete (Mb), Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Uchukuzi) ameitaka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kuendelea kuchukua hatua dhidi ya wasafirishaji na madereva wanaokiuka Sheria, Kanuni na taratibu za usafirishaji kwa magari ya abiria na magari ya mizigo.

Mhe. Mwakibete ameyasema hayo Agosti 1, 2023 alipotembelea banda la LATRA katika Maonesho ya Kimataifa ya Wakulima Nanenane viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya ambapo ameipongeza Mamlaka hiyo kwa kazi nzuri ya udhibiti wa huduma za usafiri wa abiria na mizigo kwa kutumia mifumo ya TEHAMA, kuchukua hatua stahiki kwa wasafirishaji wanaokiuka Sheria na kutoa elimu kwa Umma kwa kuwafikia wadau kwa njia mbalimbali.

“Niwapongeze LATRA kwa kuendelea kuwa Mamlaka inayoweza kudhibiti huduma za usafiri ardhini, nimeona namna ambavyo mnachukua hatua za kiudhibiti hususan katika kutoa adhabu kwa kampuni na madereva ambao hawazingatii taratibu ambazo tumejiwekea wenyewe. Hii inapunguza ajali ambazo zinaepukika, dereva anapozidisha ukomo wa mwendo au kuyapita magari mengine sehemu ambazo hairuhusiwi, anakuwa anatengeneza ajali,” alisema.

Aliongeza kuwa anafahamu wapo baadhi ya watu ambao wanachezea Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) na kusababisha gari husika kutoonekana katika mfumo, kwa kufanya hivyo anakuwa anakusudia kufanya kosa hivyo lazima mamlaka ichukue hatua kwa wasafirishaji na madereva wa aina hiyo.

Aidha ameisihi LATRA kuendelea na kazi ya kuthibitisha madereva na kusajili wahudumu kama ilivyopangwa na kuwa utekelezaji huo ni muhimu kwa kuwa unaiwezesha Serikali kusimamia huduma za usafiri na usalama wa usafiri kwa ufanisi zaidi. Mhe. Mwakibete alisisitiza kuwa Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi itaendelea kushirikiana na LATRA na wako tayari kutatua changamoto zitakazokwamisha utekelezaji wa majukumu ya mamlaka hiyo.

“Kupitia mifumo ya TEHAMA ikiwemo huu wa kufuatilia mwenendo wa mabasi inarahisisha kuchuka hatua sahihi kwa wakati, kila anayefanya makosa aadhibiwe kwa makosa yake, kwa bahati

>>> Inaendelea UK 19

>>> Inatoka UK 18

# MHE. MWAKIBETE: LATRA ENDELEENI KUCHUKUA HATUA

nzuri mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani, Mwenyekiti wetu ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, hivyo mtuletee mambo ambayo mnaona yanawapa changamoto tuyafanyie maamuzi na sisi tutaitisha vikao vya maamuzi kwa haraka," alisema.

Alisisitiza kuwa, kila mdau anapaswa kutimiza wajibu wake kuepusha ajali ili kuokoa maisha ya watanzania kwa kuwa huduma ya usafiri ni huduma ya lazima na inanafasi kubwa katika uchumi wa nchi yetu hivyo LATRA iendelee kutoa elimu katika matamasha na vyombo mbalimbali vya habari ili kufikisha elimu kwa wadau wengi zaidi.

Naye Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA Bw. Salum Pazzy alisema kuwa, LATRA imejipanga kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kipitia mifumo ya TEHAMA ambapo huduma za utoaji wa leseni, kusimamia viwango vya huduma za usafiri wa abiria na mizigo kibiashara, uthibitishaji wa madereva na usajili wa wahudumu wa vyombo vya usafiri vya kibiashara unawezeshwa kupitia mifumo mbalimbali ikiwemo mfumo wa VTS, Mfumo wa Kutahini Madereva na Mfumo tumizi wa LATRA (LATRA App) unaowawezesha abiria kujua viwango vya nauli vilivyoidhinishwa na LATRA kwa mabasi ya njia ndefu na mabasi ya mijini.

"LATRA imejipanga kutoa elimu kwa wadau na kuongeza tija kupitia mifumo ya TEHAMA ikiwemo mfumo tumizi wa LATRA ambao unapatikana katika tovuti ya LATRA na kupitia 'Play Store' ambapo abiria anaweza kuupakua kwa simu janja na kupata taarifa mbalimbali za abiria ikiwemo kujua viwango vya nauli na kuhakiki uhai wa leseni za LATRA. Kwa siku za usoni mfumo huu utamuwezesha abiria aliyekata tiketi kujua basi analotarajia kupanda lilipo," alisema.

# KAMATI YAIPONGEZA LATRA TIKETI MTANDAO

Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mhe. Miraji Mtaturu (Mb) ameipongeza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kusimamia Mfumo wa Tiketi Mtandao kwani umepunguza kero kwa abiria wa usafiri wa ardhini nchini.

Akizungumza jijini Dodoma wakati Kamati hiyo ikipokea taarifa ya Utendaji ya Mamlaka hiyo Mhe. Mtaturu amesema miongoni mwa faida za mfumo huo ni pamoja na kupunguza mianya ya uvujaji wa mapato kwani abiria ana uhuru wa kukata tiketi na hali hiyo kuruhusu mmiliki kuona idadi ya siti zilizokatwa.

"Nawapongeza sana LATRA sababu kupitia mfumo wa tiketi mtandao sasa hivi abiria anaweza kukata tiketi akiwa popote bila kulanguliwa na maajenti, lakini mfumo huu umerahisisha ukusanyaji wa mapato kwa wamiliki na Serikali sababu unaweza kuona idadi za tiketi moja kwa moja kupitia mfumo'' amesema Mhe. Mtaturu.

Aidha, Mhe. Mtaturu ameitaka LATRA kuhakikisha Kampuni ya Reli Tanzania (TRC) na Kampuni ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) zinaharakisha kuingia kwenye mfumo wa tiketi mtandao ili kuwarahisishia abiria kwani wamekuwa wakitumia muda mrefu kupanga mistari katika stesheni ili kupata tiketi.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Sekta a Ujenzi), Mhe. Atupele Mwakibete amesema Serikali imeanza kutekeleza mkakati madhubuti wa kudhibiti ajali kwa kufanya utafiti kupitia gari maalum litakalobainisha maeneo yenye changamoto za ajali ili kuja na suluhu itakayosaidia kuondoa ajali zinazosababishwa na ubovu wa barabara.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa LATRA CPA Habib Suluo ameihakikishia Kamati kuwa itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu na kufanyia kazi ushauri uliotolewa kwa lengo la kuboresha shughuli za usafirishaji ikiwemo kuendelea kuwatahini madereva ili kuhakikisha abiria wanasafiri kwa usalama.

# WASAFIRISHAJI KIGOMA WAASWA KUZINGATIA MASHARTI YA LESENI.




*CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA akizungumza na wasafirishaji Mkoani Kigoma waliojitokeza katika mkutano na wadau ulioandaliwa na LATRA ili kutoa elimu ya majukumu ya LATRA kwa mujibu wa Sheria na kupokea maoni ya wadau, Ukumbi wa Kigoma Social Hall.*

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) CPA Habibu Suluo ametoa wito kwa wasafirishaji Mkoani Kigoma kufuata misingi ya Sheria, Kanuni na taratibu za utoaji huduma hiyo ili kuweka usawa katika utoaji huduma na kuepusha malumbano yasiyo na tija katika Taifa.

CPA Suluo ameyasema hayo hivi karibuni katika mkutano na wadau ulioandaliwa na LATRA katika ukumbi wa Kigoma Social Hall ili kutoa elimu ya majukumu ya LATRA kwa mujibu wa Sheria na kupokea maoni ya wadau hao kuhusu changamoto zinazowakabili katika shughuli za usafiri na usafirishaji katika mkoa huo.

Aidha, CPA Suluo amesema kila msafirishaji anayedhibitiwa na Mamlaka anatakiwa kufuata masharti ya leseni hizo na si kufanya kadiri wanavyojiskia, "Baada ya kusikia yote tuliyoyajadili hapa nitoe wito sasa kwa wasafirishaji wote tufuate Sheria ambazo zinatuongoza katika utoaji wa huduma, magari ya kukodi ni ya kukodi na yafanye shughuli hiyo, daladala isafirishe kama daladala na hata kwa vyombo vingine kwa sababu kila mtu anapewa leseni ya usafirishaji basi kila mtu afuate masharti ya leseni aliyopewa."

Aidha CPA Suluo amemshukuru Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mazingira mazuri ya utendaji kazi anayoyaweka na kuwapongeza wadau kwa kuendelea kutoa huduma ya kusafirisha abiria na mizigo kwa niaba ya Serikali.

"Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya LATRA, Menejimenti na Wafanyakazi wa LATRA tunapenda kumshukuru Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mazingira wezeshi ya kufanyia kazi anayotuwekea, kiukweli naona kazi yangu inakuwa nyepesi, pia niwapongeza kwa jumla kwa kuendelea kutoa

>>> Inaendelea UK 21

>>> Inatoka UK 20

# WASAFIRISHAJI KIGOMA WAASWA KUZINGATIA MASHARTI YA LESENI.

huduma bila kuchoka kwani mmekabidhiwa dhamana hii kwa niaba ya serikali," ameongeza CPA Suluo.

Kwa upande wake Bw. Jahansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara amewasisitiza wasafirishaji kuwaza na kujali maslahi ya abiria ambao ndio wateja wao wakati wanapofanya biashara badala ya kuwaza faida itokanayo na biashara hiyo.

"Wote tumeshuhudia katika majadiliano yetu hakuna sehemu hata moja ambayo tumemtaja abiria, kila mmoja ametoa hoja kuvuta upande wake lakini hakuna hoja ambayo ilikuwa ni kwa ajili ya kumsaidia abiria, hivyo niwaombe mzingatie maslahi ya abiria mnapoendesha shughuli zenu na mtambue kuwa abiria mnaowahudumia ni wananchi wa hali ya chini," amesema Bw. Kahatano.

Naye Bw. Rashid Mechos, mdau wa usafiri Mkoani Kigoma ameipongeza LATRA kwa kuwafikia wadau moja kwa moja na kuwapa elimu pamoja na kusikiliza kero zinazowakabili wadau hao huku akiamini mkutano huu unakwenda kuleta matunda chanya.

"Ni mara yangu ya kwanza kushuhudia Mkurugenzi Mkuu anafika hadi kwa wadau moja kwa moja, niwapongeze sana kwa busara na hekima mliyoitumia, naamini kuwa hata pande ambazo zilikuwa zikikinzana elimu wameipata na watakwenda kubadilika," amesema Bw. Mechos.

LATRA imekuwa na utaratibu wa kukutana na wadau wa usafiri ardhini kila mara ili kutoa elimu na wakati mwingine kuwashirikisha pale Mamlaka inataka kufanya uamuzi wa jambo lenye maslahi kwa umma, hivyo ushiriki wa wadau kikamilifu ni muhimu ili kuhakikisha mawazo yao yanajumuishwa kwenye uamuzi.




***Wadau Mbalimbali Mkoani kigoma katika picha ya pamoja na CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA (aliyekaa katikati), baada ya Mkutano ulioandaliwa na LATRA ili kutoa elimu ya majukumu ya LATRA kwa mujibu wa Sheria na kupokea maoni ya wadau hao Kigoma Social Hall***



*Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi akizungumza na Wajumbe Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu waliofanya ziara ya kujifunza kuhusu jinsi LATRA inavyotekeleza majukumu yake, Septemba 9, 2023, Kituo cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS)*

# PROF. MBARAWA: KAMILISHENI TARATIBU ZA SAFARI ZA USIKU

Waziri wa Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb) amewataka wataalamu wa Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kukamilisha kwa haraka rasimu ya utaratibu wa safari za usiku ili Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) wapatiwe maelekezo ya kuanza kutoa ratiba za safari hizo.

Mhe. Prof. Mbarawa amesema hayo Septemba 9, 2023 katika Kituo cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) alipokuwa akizungumza mbele ya Mhe. Selemani Moshi Kakoso (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu pamoja na Wajumbe wa Kamati hiyo ambao wamefanya ziara ya kujifunza kuhusu jinsi LATRA inavyotekeleza majukumu yake.

Aidha, Prof. Mbarawa amesema kuwa, pamoja na Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutakiwa kuweka utaratibu utakaotumika katika kuruhusu ratiba za safari za usiku, ni muhimu kushirikisha wadau katika kufikia maamuzi ya utoaji wa ratiba hizo chini ya udhibiti wa LATRA.

Mhe. Prof. Mbarawa ameongeza kuwa, “Wakati huu ambao wataalamu wanaendelea kukamilisha taratibu hizo, LATRA na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani na Wamiliki wa Vyombo vya Usafiri ikiwa pamoja na Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) kuona uwezekano wa safari hizo kwa kuchagua njia zilizo salama na ili pengine safari zianze baina ya saa 1:00 usiku na saa 3:00 usiku.”

Ikumbukwe kuwa, Agosti 8, 2023 LATRA ilitoa rai kwa wamiliki wa mabasi ya masafa marefu nchini wenye nia ya kutoa huduma za usafiri kwa saa 24 kuwasilisha maombi yao ili muda wa kuanza safari hizo utakapoanza rasmi iwe rahisi kufahamu mahitaji halisi ikiwa ni pamoja na maeneo yanayotakiwa kupatiwa huduma hiyo.

Hatua hiyo ni katika kutekeleza agizo alilolitoa Mhe. Kassim Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Juni 28, 2023 kuhusu kuanza kwa safari za usiku kwa mabasi ya masafa marefu nchini.

# MABASI YA NEW FORCE KUANZA SAFARI SAA 9 USIKU NA 11 ALFAJIRI




Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imerudisha ratiba na leseni za mabasi 38 ya kampuni ya New Force kuanzia tarehe 11 Septemba, 2023. Mabasi hayo yataanza safari zake muda wa 9.00 usiku na saa 11.00 alfajiri.

Hayo yamebainishwa na Bw. Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara kutoka LATRA kwenye mkutano na waandishi wa habari uliofanyika Septemba 8, 2023 katika ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam.

Bw. Kahatano amesema kuwa LATRA imefikia uamuzi huo baada ya kujiridhisha kuwa kampuni hiyo imetekeleza maelekezo iliyowapatia hapo awali ikiwemo kuhakikisha wanazingatia muda wa kuanza safari, kutafuta mshauri mwelekezi kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa uongozi wa kampuni na madereva kuhusu Sheria za Usalama Barabarani na Udereva wa Kujihami na udhibiti wa uchovu pamoja na kuhakikisha kuwa madereva wote wanasajiliwa kwenye mfumo wa ufuatiliaji mwenendo wa magari (VTS), kuwa na i-button na kusajiliwa kwenye mfumo wa uthibitisho wa madereva.

"Tumepokea taarifa ya mafunzo yaliyotolewa kwa madera 50 wa kampuni hiyo kwa kuona vyeti vya kuhitimu mafunzo, tumepokea orodha ya wadhamini wa madereva hao kuwa wamesoma wameelewa na watazingatia Sheria zote za Usalama Barabarani katika kutoa huduma za usafirishaji abiria na tumefuatilia kwenye mfumo wa VTS mabasi yote ya kampuni hiyo kwa kipindi chote cha adhabu na kujiridhisha kuwa uvunjifu wa ratiba kwa kutoka kabla ya muda na mwendo kasi umedhibitiwa. Hii ni dalili njema kwa uongozi na madera wa kampuni hii kutii Sheria," ameeleza Kahatano.

Vilevile ameeleza kuwa, kutolewa kwa ruhusa hiyo iwe ni fundisho kwa kampuni ya New Force na wasafirishaji wote wanaokiuka Sheria, Kanuni na taratibu za Usalama Barabarani na Mamlaka haitasita kuchukua hatua stahiki kwa yeyote atakayevunja Sheria na taratibu zilizowekwa.

Naye Bw. Masumbuko Masuke, Meneja wa Kampuni ya New Force amesema, "Tunaishukuru LATRA na Jeshi la Polisi kwa kutupatia elimu ya Usalama Barabarani na tunaahidi kutekeleza Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo. Tunawaomba radhi abiria wetu kwa yote yaliyotokea na niwahakikishie kuwa kwa sasa tumebadilika, tutazingatia yote tuliyoelekezwa."



# DKT. ALLY POSSI: TRC, TAZARA BORESHENI MIUNDOMBINU YA RELI

Dkt. Ally Possi, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Uchukuzi ameagiza Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia (TAZARA) kurejesha upya alama za usalama wa reli kwa maeneo yote ambayo alama zimeondolewa au kuharibika.

Ameyasema hayo Oktoba 13, 2023 katika kilele cha Maadhimisho ya wiki ya Usalama wa Reli yaliyofanyika nchi za Jumuiya ya Mashirika ya Reli ya Kusini mwa Afrika (SARA) ambapo kwa upande wa Tanzania, maadhimisho haya yalifanyika kitaifa mkoani Tabora.

Dkt. Possi amezitaka taasisi zinazo simamia usafiri wa reli kuboresha miundombinu ya reli iliyoharibika ili kuhakikisha uwepo wa usalama na Usafiri bora kwa wananchi.

"Boresheni miundombinu hasa katika sehemu ambazo zimeharibiwa na wananchi na wamekuwa wakisababisha hasara kwa Serikali, Kwa wakandarasi na taasisi zetu sote tunapojenga miundombinu yetu tuhakikishe tunazingatia na kuboresha usalama wa wananchi" Amesema Dkt. Possi.

Aidha, amewasihi watanzania wote wawe walinzi wa miundombinu ya reli kwa maendeleo yetu wote, kwa kuwa wapo watu au kundi la watu wanaohujumu miundombinu ya reli na huo ni uhalifu, na kuwataka wananchi kutoa taarifa haraka kwa mamlaka za Serikali na Jeshi la Polisi

"Nitoe rai kwa wananchi na sisi sote kwa ujumla kutunza miundombinu, kwani tunapo iharibu ndipo tunapo hatarisha pia usalama wa usafiri wetu wa reli hivyo basi ukiona mtu au kundi la watu linahujumu miundombinu ya reli, huo ni uhalifu, na pia ni uhujumu uchumi, na kamwe Serikali hatuwezi kufumbia macho suala hili" Amesema Dkt. Possi .

Vilevile amesisitiza kuwa wananchi wanaoishi maeneo ya karibu na reli waendelee kukumbushana umuhimu wa kutunza na kulinda miundombinu na mazingira ya reli.

"Naomba nitumie fursa hii kutoa wito kwa wananchi wanaoishi maeneo inakopita reli na watanzania wote kwa ujumla, waendelee kukumbushana umuhimu wa kutunza na kulinda

>>> Inaendelea UK 25

>>> Inatoka UK 24

# DKT. ALLY POSSI: TRC, TAZARA BORESHENI MIUNDOMBINU YA RELI

miundombinu ya reli pamoja na mazingira yake kwa maendeleo ya nchi yetu, kwa kuunga mkono juhudi za dhati za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika uwekezaji mkubwa unaoendelea kwenye sekta ya reli ili kuboresha miundombinu ya reli zetu na kukuza uchumi wa Tanzania" Amesema Dkt. Possi.

Vilevile ameilekeza TRC kukamilisha kwa wakati ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kwa kipande kinachoanzia Dar es Salaam mpaka Morogoro na Morogoro mpaka Makutupora kwa sababu ujenzi umechelewa sana kukamilika na wananchi wanahamu ya kupanda treni kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora.

"Nitoe maelekezo kwa TRC kuhakikisha kipande cha kwanza na cha pili kinakamilika kwa wakati, kwa sababu imechukua muda mrefu na wananchi wanahamu ya kupanda treni kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora" Ameeleza Dkt. Possi.

Aidha Dkt. Possi ametoa taarifa kwa wananchi kuwa Wizara ya Uchukuzi inashirikiana na TAZARA katika hatua ya kuboresha miundombinu ya TAZARA kwa dhumuni la kukuza uchumi na kuboresha utoaji huduma kwa kuwa itasaidia usafirishaji wa mizigo hususan kutoka bandari ya Dar es Salaam mpaka nchi jirani.




"Nitoe taarifa kwa wananchi kuwa Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na TAZARA tupo katika hatua ya kuboresha miundombinu na wote tunafahamu sekta ndogo ya reli ni kichocheo cha uchumi lakini pia ni kichocheo kikubwa cha utoaji huduma kwani reli itasaidia usafirishaji wa mizigo hususan kutoka bandari yetu ya Dar es Salaam mpaka nchi jirani na ndani ya nchi yetu, wananchi watakuwa wanapata huduma ya usafiri wa reli kwa raha. Kwa bahati nzuri Serikali imepitisha bajeti ya kuendeleza miundombinu hii pamoja na kuhakikisha usalama wa wananchi unaendelea kutunzwa" Amesema Dkt. Possi.

Kwa upande wake Prof. Ahmed Mohamed Ame, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Amesisitiza juu ya matumizi ya mifumo ili kuongeza ufanisi katika sekta ya usafirishaji kwa kuongeza usalama na kukuza uchumi katika Usafiri wa reli.

>>> Inaendelea UK 26

>>> Inatoka UK 25

# DKT. ALLY POSSI: TRC, TAZARA BORESHENI MIUNDOMBINU YA RELI

"Nipende kusisitiza juu ya mifumo katika kuongeza ufanisi, hii ni pamoja na Mfumo wa kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) na mfumo wa Tiketi Mtandao ili kuongeza usalama na kuhakikisha ufanisi wa kiuchumi katika reli zetu na yote haya yanawezekana iwapo tutaamua kubadilika" Amesema Prof. Ame.

"Napenda kuwakumbusha waendeshaji wa huduma za reli nchini, TRC na TAZARA kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za uendeshaji wa huduma za reli ili kuhakikisha usalama na kutoa huduma kwa ufanisi ikiwemo treni kufika vituoni kwa wakati" Ameongeza Prof. Ame.

Vilevile Prof. Ame amewataka vijana waliofuzu mafunzo yaliyoandaliwa na ofisi ya Mkuu wa Kikosi cha Usalama barabarani Mkoa wa Tabora kutengeneza vikundi vya ushirika ili waweze kupeana elimu wenyewe kwa wenyewe na LATRA itawatumia kama waratibu wake kwa kutoa leseni kwa vijana wenye bodaboda mkoani Tabora.

Naye Mha. Hanya Mbawala Kaimu Mkurugenzi wa Udhibiti Usafiri wa Reli kutoka LATRA, Ameeleza kuwa LATRA inajukumu kubwa sana katika kudhibiti Usafiri wa Reli kwa kutoa ithibati ya vitendea kazi, miundombinu na mabehewa ya treni ili kuhakikisha reli inafanya kazi kwa usalama kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizowekwa.

"Wananchi wengi wanaiona LATRA kwa upande wa Barabara tu lakini jukumu kubwa ni katika usafiri wa reli kwa kuhakikisha inafanya kazi kwa usalama kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu zilizowekwa kwa kutoa ithibati ya vitendea kazi, miundombinu na mabehewa, haya yote ni kuhakikisha Usafiri salama kwa wananchi pamoja na kukuza uchumi kwa ujumla" Amesema Mha. Mbawala.

"Hivi karibuni tutaanza majaribio ya Reli ya Kisasa (SGR) na tunatoa wito kwa wananchi wasiingie katika uzio wa SGR kwa sababu watapata madhara makubwa ambayo yanaweza kugharimu maisha yao" Ameongeza Mha. Mbawala.

Maadhimisho haya ya wiki ya Usalama wa Reli yenye kaulimbiu ya ***"usalama unaanza na wewe, chukua tahadhari"*** yamefanikisha utoaji wa elimu kwa makundi mbalimbali ya wananchi wa Tabora na taasisi zinazosimamia usafiri wa reli zinatoa wito kwa wananchi na madereva wa vyombo vya moto wanatakiwa kuchukua tahadhari endelevu wanapotumia miundombinu ya reli.



# SAFARI SAA 24 RUKSA KUANZIA OKTOBA 1, 2023




Serikali imetangaza rasmi kuanza kutolewa kwa ratiba za mabasi ya abiria kusafiri kwa saa 24 kuanzia Oktoba 1, 2023

Kauli hiyo imetolewa na Mhe. Jumanne Sagini (Mb), Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika katika ukumbi wa Golden Tulip jijini Dar es Salaam, Septemba 29, 2023.

Mhe. Sagini amesema kuwa, Serikali inataka kuona usafiri wa saa 24 unakuwa salama na wenye ufanisi huku akiitaka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kutoa ratiba za saa 24 kwa kuwashirikisha watoa huduma na kuhakikisha Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) unafanya kazi muda wote.

Akieleza sababu za kuanza kwa huduma hizo za saa 24, Mhe Sagini ameeleza kuwa, tathmini iliyofanyika imeonesha kuwa udhibiti wa hali ya usalama umeimarika kupitia Jeshi la Polisi, wananchi wamebadilika kitabia na kuanza kuhifadhi pesa zao benki hivyo hawatembei na pesa taslimu, huduma za mawasiliano ya simu zimeboreshwa, LATRA imesimika mfumo madhubuti wa kufuatilia mwenendo wa magari (VTS), miundombinu ya barabara imeimarika na wasafirishaji wapo tayari kufuata Sheria, Kanuni na taratibu zilizowekwa,

Aidha, Mhe. Sagini ametoa maelekezo mahususi kwa wasafiri na wasafirishaji, " Wamiliki wa mabasi wanatakiwa kufuata Sheria, Kanuni na taratibu kwa mujibu wa leseni zao na Madereva wa mabasi wanapaswa kuthibitishwa na LATRA kwa mujibu wa Kanuni zilizopo"

Vilevile amesema kuwa, "TAMISEMI ihakikishe kunakuwepo na huduma za msingi hasa katika stendi za mabasi na Jeshi la polisi liendelee kulinda watu na mali zao wakati wote, usiku na mchana na kuimarisha doria katika maeneo ya stendi, barabara kuu na barabara za mikoa na kuhakikisha Sheria za Usalama Barabarani zinazingatiwa na kila mdau."

Naye Bw. Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara kutoka LATRA amesema Mamlaka imejipanga kikamilifu kusimamia safari za saa 24 kwa kuweka mikakati thabiti itakayowezesha safari

>>> Inaendelea UK 28

>>> Inatoka UK 27

# SAFARI SAA 24 RUKSA KUANZIA OKTOBA 1, 2023

hizo kuwa na tija katika maendeleo ya Taifa huku usalama ukiwa ni kipaumbele.

"Kwa upande wetu tunayo nguvu ya kutosha ili kusimamia eneo hili, hivyo niwakaribishe wasafirishaji ambao wana nia ya kufanya safari hizi watume maombi, mpaka sasa tuna maombi ya makampuni 7 yanayotaka kufanya safari hizi. Katika kusimamia huduma hizi, wasafirishaji watasaini tamko ambalo litaelezea ulazima wa madereva kuwa wamesajiliwa, kuwa na mtu maalumu ambaye atasimamia magari haya usiku, taarifa sahihi za abiria kuwepo kwenye mfumo wa Tiketi Mtandao pamoja na kuweka utambulisho maalum wa mizigo ya abiria," amesema Bw. Kahatano.

Kwa upande wake, SACP Ramadhani Ng'anzi, Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani amesema kuwa Jeshi hilo litaendela kuhakikisha usalama wa raia na mali zao mahali popote ili kufanya nchi iwe salama.

Safari za saa 24 zilisitishwa kwa agizo la Serikali mwaka 1994 kutokana na sababu mbalimbali kama vile; hali ya usalama wa raia na mali zao, miundombinu mibovu na ajali zilizokuwa zinasababisha madhara makubwa kwa binadamu. Hata hivyo, Serikali kupita LATRA ilianza kuruhusu safari kuanzi saa 11 alfajiri na baadae saa 9 alfajiri ili kujiridhisha na udhibiti wa safari hizi na hatimaye safari za saa 24 zimeruhusiwa. Umetolewa wito kwa watumiaji wa huduma za usafiri nchini (wasafirishaji na abiria) kuzingatia Sheria za Usalama Barabarani ili kuhakikisha faida zilizotazamiwa kwenye safari hizi zinafikiwa kikamilifu.

# LATRA YAJIKITA KUSIMAMIA USAFIRI SALAMA

Mkuu wa Wilaya ya Uyui, Mhe. Zakaria Saili Mwansasu, ameipongeza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kuendelea kusimamia Sheria na Kanuni za usafiri ardhini, kuboresha huduma za usafiri nchini na kupunguza kwa kiasi kikubwa ajali na maafa yatokanayo na matumizi mabaya ya vyombo vya usafirishaji.

Ameyasema hayo tarehe 9 Oktoba, 2023 kwa niaba ya Mhe. Balozi, Dkt. Batilda Buriani, Mkuu wa Mkoa wa Tabora katika hafla ya ufunguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Usalama wa Reli yanayofanyika nchi za Jumuiya ya Mashirika ya Reli ya Kusini mwa Afrika (SARA) ambapo kwa upande wa Tanzania, maadhimisho haya yanafanyika Kitaifa Mkoani Tabora.

Aidha, amesisitiza kufanyika maboresho ya mfumo wa Tiketi Mtandao ili kuongeza ufanisi wa huduma za usafiri wa abiria wa treni ikiwa ni pamoja na kuzuia mianya ya upotevu wa fedha za Serikali katika huduma za reli.

"Naomba nitumie fursa hii kuwapongeza LATRA kwa hatua wanazochukua na kulielekeza Shirika la Reli Tanzania (TRC) kuboresha Mfumo wa Tiketi Mtandao kwa abiria wa treni ili wajikatie tiketi zao wenyewe popote walipo kwa njia ya mtandao" Amesema Mhe. Mwansasu.

Aliongeza kuwa, maelekezo hayo ni muendelezo wa maagizo ya Serikali yaliyotolewa na Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi, alipokuwa akizindua Bodi ya Wakurugenzi ya TRC hivi karibuni.

"Haya pia ni maagizo ya Serikali yaliyosisitizwa na mambo haya yamewezekana kwenye usafiri wa mabasi zaidi ya 8,500 nchini, hatuoni sababu ya kutowezekana kwa TRC. Kwa ujumla, tunaona mabadiliko makubwa katika sekta ya reli yanakuja hapa Nchini. Kwa hili nawapongeza sana LATRA. Endeleeni kufanya kazi kwa kuzingatia Sheria, na kila mmoja atimize wajibu wake ili watanzania

>>> Inaendelea UK 29

>>> Inatoka UK 28

# LATRA YAJIKITA KUSIMAMIA USAFIRI SALAMA

wafurahie huduma bora na salama za usafiri wa reli," aliongeza Mhe. Mwansasu.

Vilevile, Mhe. Mwansasu amewasisitiza wananchi kutembelea maonesho hayo ili waweze kupata elimu inayohusiana na usalama wa reli pamoja na kulinda miundombinu ya reli nchini huku wakizingatia kauli mbiu ya mwaka huu inayosema "***Usalama Unaanza na Wewe Chukua Tahadhari"*** kwa kuwa Serikali inaendelea kuhakikisha usafiri wa reli unakuwa salama kwa kushirikiana na wananchi.

"Tuwe walinzi wa miundombinu kwa maendeleo ya nchi yetu na nisisitize katika maeneo yote ambayo alama za usalama wa reli zimeondolewa ziwekwe upya mapema kwa ajili ya kuimarisha usalama wa usafiri wa reli, abiria na mali zao kwa ujumla" alisisitiza Mhe. Mwansasu.

Kwa upande wake Prof. Ahmed Mohamed Ame, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi LATRA amemshukuru Mhe. Mwansasu kwa pongezi alizozitoa na kuahidi kuwa LATRA itaendelea kuboresha udhibiti wa huduma za usafiri ili kuongeza tija na kukuza uchumi.

"Nipende kuwasihi TRC, TAZARA na LATRA kusimamia vizuri usalama wa reli mpaka kufikia asilimia 100, kuwahakikishia na kuwaaminisha wananchi na wadau wote kuwa usafiri wa reli ni salama na haraka ndipo tutakapo kuza uchumi wetu," amesema Prof. Ame.

Naye, CPA Habibu J. Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, amewapongeza madereva bodaboda wa mkoani Tabora, waliofuzu mafunzo ya udereva yaliyowezeshwa na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani na kupatiwa vyeti katika hafla hiyo ambapo ameahidi kutoa ushirikiano kwa madereva hao na kuwasihi vijana wengine wajitokeze kupata mafunzo.

"Sisi LATRA tunafarijika sana na juhudi hizi za madereva wa bodaboda zinazorahisisha udhibiti, tunawasihi kujiunga katika umoja wa vyama vya ushirika kama SACCOS na LATRA itawatambua na tunaahidi kuwapa vitendea kazi ili waweze kujidhibiti wenyewe na kujiongezea kipato," amesema CPA Suluo.




*Mhe. Zakaria Saili Mwansasu, Mkuu wa Wilaya ya Uyui akizungumza na wananchi waliohudhuria hafla ya ufunguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Usalama wa Reli yanayofanyika nchi za Jumuiya ya Mashirika ya Reli ya Kusini mwa Afrika (SARA) ambayo Kitaifa yamefanyika Mkoani Tabora, Oktoba 9, 2023*

# TRC KUSHINDANISHWA NA SEKTA BINAFSI KUTOA HUDUMA ZA USAFIRI WA RELI



Dkt. Ally Possi, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Uchukuzi ameitaka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kuharakisha kuandaa miongozo na leseni zitakazotolewa kwa wadau wa sekta binafsi watakaotumia miundombinu ya reli mara baada ya Kanuni za kuruhusu wawekezaji binafsi kwenye miundombinu hiyo kukamilika.

Dkt. Possi ameyasema hayo alipofungua mkutano wa kupokea maoni ya wadau kuhusu Rasimu za Kanuni za Watoa Huduma Binafsi za Usafiri wa Reli za Mwaka 2023, uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Chuo cha Utalii jijini Dar es Salaam Oktoba 16, 2023.

"LATRA muanze kuandaa miongozo na taratibu za kupata leseni kwa haraka na kwa uwazi bila kusahau eneo hili linaenda kuchochea ushindani kwa Shirika la Reli Tanzania (TRC). Lengo ni kutimiza dhima ya Serikali ya kuongeza ufanisi katika usafiri wa reli na kuboresha utoaji wa huduma," amesema Dkt. Possi.

Vilevile Dkt. Possi ameongeza kuwa, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefungua milango kwa sekta binafsi katika kuchangia uchumi wa nchi kwa kuwa sekta hizo zina uwezo madhubuti wa kushiriki katika utoaji wa huduma ya usafirishaji kwa njia ya reli.

Aidha, amesema kuwa, ni wakati mwafaka kwenda na kasi ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha uwekezaji na maboresho yanayoendelea katika Bandari ya Dar es Salaam, yanatuwezesha kuondosha mizigo kwa haraka kwa kupitia Reli.

Dkt. Possi ameongeza kuwa, kuwepo na ushindani wenye usawa kwa TRC na sekta binafsi itasaidia TRC kuongeza kasi ya uboreshaji wa huduma, "Nia yetu sisi mizigo isafiri, abiria wahudumiwe na Bandari yetu inufaike na kasi ya kukuza uchumi wetu iongezeke," amesema Dkt. Possi.

Aidha Dkt. Possi ameitaka TRC kutafuta mshauri wa kitaalamu kwa haraka atakayeweza kuwapa maoni mazuri zaidi kuhusu kuwezesha

>>> **Inaendelea UK 31**

>>> Inatoka UK 30

# TRC KUSHINDANISHWA NA SEKTA BINAFSI KUTOA HUDUMA ZA USAFIRI WA RELI

watoa huduma binafsi kwenye miundombinu ya reli kulingana na mazingira ya nchi yetu.

Kwa upande wake CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, ameeleza kuwa LATRA kama mdhibiti itasimamia vyema utoaji wa huduma za usafiri wa reli kwa sekta binafsi ili kuongeza ufanisi kama ilivyoelekezwa na Wizara ya Uchukuzi, na amewakaribisha wadau kutoa maoni yao ili kuboresha Kanuni hizo.

"Waziri wa Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa (Mb) ametoa maelekezo kwetu kama mdhibiti tuhakikishe tunatoa leseni kwa watu binafsi kutumia njia ya TRC kutoa huduma. Na tumefanya tathmini kwa mwaka 2019 hadi 2023 na kuona reli yetu ina uwezo mkubwa wakusafirisha mizigo zaidi kutoka bandari yetu na kwenda sehemu mbalimbali hivyo niwakaribishe wadau wote watoe maoni ambayo yatasaidia kuleta kanuni zenye tija na zinazoendana na uhalisia" ameeleza CPA Suluo.

Naye Mkurugenzi Msaidizi wa huduma za usafiri wa reli kutoka Wizara ya Uchukuzi Bw. Benjamin Mbimbi ameeleza kuwa, Serikali itaweka utaratibu maalum ambao utawezesha watoa huduma binafsi kutekeleza majukumu yao na Serikali kupata mapato yake.

"Serikali imetoa fursa kwa sekta binafsi kushiriki katika kutoa huduma kwa kununua mabehewa na vichwa vya treni na kupitia Kanuni hizi kutakuwa na utaratibu maalum wa kulipia ada ya kutumia njia ya treni ya TRC, huku jukumu la kumiliki na kuboresha miundombinu litabaki kuwa la Serikali, hii pia itasaidia katika kuongeza kasi ya uchumi katika sekta ya reli nchini" ameeleza Bw. Mbimbi.

Ili kuboresha Kanuni za usafirishaji kwa njia ya reli wadau wamepewa siku 14 kuwasilisha maoni yao kwakuwa ni muhimu katika kuboresha utoaji huduma wa Usafiri wa reli kwa wananchi.

# CPA SULUO: SERIKALI YA AWAMU YA SITA IMETUPAISHA KIUTENDAJI

CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amesema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeiwezesha LATRA kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi na hivyo imeipa mafanikio makubwa katika utekelezaji wa majukumu yake.

CPA Suluo amebainisha hayo kwenye Mkutano na Wahariri wa Vyombo vya Habari uliofanyika Oktoba 19, 2023 katika ukumbi wa mikutano wa Golden Jubilee, jijini Dar es Salaam na ameeleza kuwa mafanikio ya LATRA yamejidhihirisha katika sekta tatu zinazodhibitiwa na Mamlaka hiyo ambayo ni sekta ya usafiri wa barabara, usafiri wa reli na usafiri wa waya.

Aidha, CPA Suluo amesema kuwa, katika usafiri wa barabara, kwa kipindi cha mwaka 2020/21 hadi 2022/23, idadi ya leseni za usafirishaji iliongezeka kutoka leseni 230,253 hadi leseni 284,158 ikiwa ni sawa na ongezeko la leseni 44,205 ambayo ni ongezeko la asilimia 18.4.

"kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)( b) cha Sheria ya LATRA, Mamlaka inao wajibu wa kutoa, kuhuisha, kusitisha na kufuta leseni za usafirishaji, hivyo Mamlaka hutoa leseni kila mwaka kwa vyombo vya usafiri kibiashara. Leseni hizi hutolewa baada ya mtoa huduma kukidhi masharti yanayotakiwa kwa aina ya huduma husika. Leseni hizi hutumika kutambua idadi ya watoa huduma wanaodhibitiwa," ameeleza CPA Suluo.

Vilevile amesema kuwa, Mamlaka ina jukumu la kusajili wahudumu na kuthibitisha madereva wa vyombo vinavyodhibitiwa kwa lengo la kupata madereva wenye sifa na weledi kuendesha magari yanayotoa huduma kwa usafiri wa umma kwa kupima umahiri wao hasa maarifa waliyopata ili kuimarisha usalama, "Hadi, kufikia Septemba 30, 2023, madereva 17,990 wamesajiliwa na kuingiza taarifa zao

>>> Inaendelea UK 32

>>> Inatoka UK 31

# CPA SULUO: SERIKALI YA AWAMU YA SITA IMETUPAISHA KIUTENDAJI

kwenye kanzidata ya Mamlaka ambapo madereva 1,617 wamethibitishwa baada ya kufaulu mtihani wa kuthibitishwa na LATRA. Miongoni mwa madereva hawa madereva wa mabasi wapatao 645 wamesajiliwa kwenye mfumo wa kufuatilia mwenendo wa mabasi (VTS) na kupatiwa kitufe maalumu cha utambulisho (identification button, i-button). Matumizi ya kitufe hicho ni kurahisisha utambuzi wa dereva anayeendesha gari kwa wakati husika kupitia mfumo wa VTS."

Katika Usafiri wa Reli, CPA Suluo ameeleza kuwa Mamlaka, imeendelea kutoa mafunzo kazini kila mwaka kwa Wafanyakazi Muhimu wa Usalama katika uendeshaji wa reli (Safety Critical Workers) kwa TAZARA na TRC ili kuwaongezea ujuzi wa kutimiza majukumu yao kwa weledi na kwa mwaka wa fedha 2023/2024 LATRA imepanga kuhakikisha usalama wa abiria na mizigo unazingatiwa katika usafiri wa reli.

"Mafunzo ya aina hii husaidia kuwajengea uwezo wafanyakazi hao muhimu kuzuia ajali zitokanazo na makosa ya kibinadamu (Human Errors). Tathmini inaonesha kwamba, makosa ya kibinadamu katika uendeshaji wa shughuli za reli huchangia zaidi ya asilimia 85% ya ajali zote za treni kwa TRC na TAZARA. Hivyo, mafunzo hayo yatasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza ajali zinazosababishwa na makosa ya kibinadamu," amefafanua CPA Suluo.

Aidha, CPA Suluo ameeleza kuwa, LATRA imepiga hatua kubwa katika matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambapo Mamlaka inatumia mifumo mbalimbali ikiwemo Mfumo wa Usimamizi wa Shughuli za Kiudhibiti (RRIMS), Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS), Mfumo wa Tiketi Mtandao, Mfumo Tumizi wa LATRA (LATRA App), Mfumo wa e-Mrejesho pamoja na Mfumo wa Taifa wa Ununuzi wa Umma wa Kieletroni (NeST).

CPA Suluo amesema kuwa, Mfumo wa RRIMS unaopatikana kwa anwani ya https://rrims.latra.go.tz/login unamwezesha mteja kufanya maombi ya leseni ya usafirishaji kutokea mahali popote alipo na maombi yote yanayowasilishwa yanafanyiwa kazi siku hiyo na kuhakikisha anapata leseni chini ya saa 24. "RRIMS imeunganishwa na mifumo ya taasisi nyingine za Serikali kama vile TRA, TIRA, NIDA, GePG na BRELA na pia imeunganishwa na mifumo ya wadau wengine kama vile watoa huduma wa tiketi mtandao ili kurahisisha utoaji huduma za Mamlaka kwa wananchi."

Vilevile amesema LATRA imeanza kutumia Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) tangu mwaka 2017 na hadi sasa, zaidi ya magari




*CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) akizungumza na wanahabari katika Mkutano na Wahariri wa Vyombo vya Habari uliofanyika Oktoba 19, 2023 katika ukumbi wa mikutano wa Golden Jubilee, jijini Dar es Salaam*

>>> Inaendelea UK 33

>>> Inatoka UK 32

# CPA SULUO: SERIKALI YA AWAMU YA SITA IMETUPAISHA KIUTENDAJI

9,420 yameunganishwa na mfumo huu ambapo, magari 7,620 yapo hai na yaendelea kutoa taarifa kupitia mfumo huu. “Mfumo umesaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa ajali za barabarani zinazotokana na mwendokasi, umepunguza madhara ya ajali zinazotokana na mwendokasi na umerahisisha uchunguzi wa ajali pale zinapotokea.”

Ameelezea mifumo mingine ni Mfumo wa Tiketi Mtandao ambao umesaidia kudhibiti upandishaji holela wa nauli. Mfumo Tumizi wa LATRA (LATRA App) unaopatikana ‘Play Store’ kwenye simu zote za Android na unamwezesha mwananchi kupata taarifa za nauli za mabasi ya masafa marefu na mabasi ya mijini na Mamlaka inaendelea kuboresha huduma za mfumo huo ili kuwezesha abiria kutambua mwendo kasi wa gari.

CPA Suluo amesema Mamlaka pia imejiunga na inatumia Mfumo wa Serikali wa e-Mrejesho unaopatikana kupitia https://emrejesho.gov.go.tz kwa ajili ya kupokea Malalamiko, Mapendekezo, Pongezi au Maulizo na hivyo amewasihi wananchi kutumia mfumo huo kuwasilisha maoni yao ambayo yatafanyiwa kazi ndani ya siku 21. Pia LATRA inatumia Mfumo wa Taifa wa Ununuzi wa Umma wa Kieletroni (NeST) kwa ajili ya kutangaza na kuchakata zabuni mbalimbali na hivyo amewashauri wazabuni wajisajili kwenye mfumo huo ambao unapatikana kwenye tovuti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) ili kuweza kushiriki kwenye zabuni Serikalini.

CPA Suluo ameeleza kuwa, LATRA pia inajivunia kutekeleza dhana ya ushirikishaji wa wadau kwa vitendo ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/23, LATRA ilifanya jumla ya mikutano ya wadau 36 ikiwemo mikutano 9 ya kupokea maoni kuhusu mapitio ya nauli, mikutano 6 ya mabadiliko ya kanuni, mikutano 6 ya kutoa elimu kuhusu masuala kiudhibiti, mikutano 7 ya kutunza mazingira na kuimarisha usalama wa usafiri ardhini. Aidha, Mamlaka ilifanya mikutano 8 kwa ajili ya kuzitafutia ufumbuzi kero mbalimbali kwenye usafiri wa barabara na reli.

# MHE. KIHENZILE AIPA TANO LATRA KWA KUTUMIA MFUMO WA VTS

Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb) Naibu Waziri wa Uchukuzi ameipongeza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kutumia Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza ajali za barabarani na athari zitokanazo na ajali.

Mhe. Kihenzile ameyasema hayo Novemba 20, 2023, alipotembelea ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam na Kituo cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) kilichopo Mikocheni Jijini Dar es Salaam na kujionea shughuli mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka ikiwemo utoaji wa leseni pamoja na usajili na uthibitishaji wa madereva wa vyombo vya moto kibiashara.

“Napenda kuipongeza LATRA kwa kazi nzuri na nimefurahishwa kuona jinsi nchi yetu ilivyopiga hatua kubwa katika teknolojia ya kudhibiti magari kupitia mfumo wa VTS, kwa kiwango kikubwa umepunguza ajali za barabarani ukilinganisha na kipindi cha nyuma ambapo VTS ilikuwa bado haijaanza kutumika nchini,” alisema Mhe. Kihenzile.

Ameongeza kuwa, “Ufanisi wa mfumo huo ndio uliifanya Serikali iruhusu magari ya abiria kufanya kazi saa 24 kwa kuwa iliamini upo mfumo unaofanya kazi usiku na mchana hata kama askari wa usalama barabarani hawapo.”

Vilevile, amewataka madereva kuendelea kujitokeza kwa wingi kusajiliwa na kuthibitishwa na LATRA na kutii Sheria za Usalama Barabarani ikiwemo kuacha kuingilia mfumo wa VTS ili kuepusha ajali na vifo visivyokuwa vya lazima.

“Napenda kutoa wito kwa madereva kuendelea kutii Sheria za Usalama Barabarani na wawaonee huruma wananchi wanaopoteza maisha bila sababu za msingi kwa kuwa tunapoteza nguvu kazi ya Taifa, nawasihi madereva wajitokeze kusajiliwa na kuthibitishwa na LATRA ili kuwatambua madereva wanaokuwa safarini wakiendesha vyombo

>>> Inaendelea UK 34



*Prof. Ahmed Mohamed Ame, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi LATRA akimuelezea Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb) Naibu Waziri wa Uchukuzi namna LATRA inavyotumia Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) kudhibiti usalama wa usafiri nchini, katika ziara ya Mhe. Kihenzile Ofisi za LATRA Dar es Salaam, Novemba 20, 2023,*

>>> Inatoka UK 33

# MHE. KIHENZILE AIPA TANO LATRA KWA KUTUMIA MFUMO WA VTS

vya moto kibiashara na kupunguza changamoto zinazojitokeza barabarani," alieleza Mhe. Kihenzile.

Kwa upande wake, Prof. Ahmed Mohamed Ame, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi LATRA, amemshukuru Mhe. Kihenzile kwa kuitembelea ofisi ya LATRA Mkoa wa Dar es Salaam na amemuahidi kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kuwezesha mfumo wa VTS kutuma namba ya malipo (control number) moja kwa moja pale dereva anapokiuka Sheria kama ilivyokuwa hapo awali.

"Mfumo unaweza kufanya mambo mengi ikiwemo kutuma moja kwa moja namba ya malipo kwa kutoa adhabu moja kwa moja kwa madereva wanaokiuka Sheria za barabarani na kwa sasa tunaendelea kuzungumza na wenzetu Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani ifike mahala mfumo uweze kufanya hivyo kwasababu ulishawahi kufanya hivyo huko nyuma.

Mfano katika ziara hii ya Mhe. Kihenzile niliangalia kwenye mfumo wa VTS na kuona dereva mmoja ametumia kifaa cha 'i - Button' kuwasha magari matatu kwa pamoja na kuwapa madereva tofauti kuendesha lakini sisi mfumo ulitujulisha," alisema Prof. Ame.

Naye Bw. Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara kutoka LATRA alieleza kuwa, usajili wa madereva unaenda vizuri, hadi sasa madereva 2,757 wameshafanya mtihani wa kuthibitishwa na LATRA na madereva 1,817 wamefaulu na waliofeli wanayo fursa ya kurudia mtihani huo.

"Kutokana na matukio ya ajali yanayojitokeza tumefanya tathmini na tumepata faraja kuona kwamba tangu mwezi Septemba hadi sasa wale madereva wachache tuliowathibitisha wanafanya vizuri barabarani na kubaini wachache ndio wanaokiuka Sheria lakini bado tunaendelea kuwafuatilia kila siku hususan kwenye safari za usiku, itambulike kuwa katika kuchukua hatua za kisheria haijalishi dereva awe amethibitishwa au hajathibitishwa iwapo atabainika kuvunja Sheria tutampatia adhabu," alieleza Bw. Kahatano.




*LATRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wakiendelea na tathmini ya hali ya usafiri wa vyombo vya moto kibiashara katika kipindi cha Siku Kuu za mwisho wa mwaka.*

*Wadau mbalimbali Mkoani Kigoma waliohudhuria Mkutano ulioandaliwa na LATRA ili kupokea maoni ya wadau hao katika ukumbi wa Kigoma Social Hall*






*Mdau wa Usafiri Ardhini akipatiwa elimu ya shughuli za udhibiti zinazotekelezwa na LATRA kwa mujibu wa Sheria, katika maonesho ya 16 ya wadau wa Sekta ya Uchukuzi, Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC)*



**Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano cha Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kikiongozwa na Bodi ya Wahariri**

**Mwenyekiti:** CPA HABIBU SULUO | **Mhariri Mkuu:** SAMUEL KEENJA | **Wahariri Wasaidizi:** SALUM PAZZY, MAMBWANA JUMBE | **Waandishi:** MAMBWANA JUMBE, MARIAM NINA, DEUSDEDITY MASEMBA | **Msanifu Picha:** IBRAHIM SAID | **Wapiga Picha:** IBRAHIM SAID, DEUSDEDITY MASEMBA | **Wasanifu Jarida:** IBRAHIM SAID, DEUSDEDITY MASEMBA